



Global
Soil Week

VIDOKEZO VYA MWONGOZO WA JUMUIYA VYA KUKODISHA ARDHI

WADI YA ISUKHA YA MAGHARIBI, GATUZI - NDOGO LA SHINYALU,
KAUNTI YA KAKAMEGA

Doreen Magotsi | William Onura Akwany | Linet Khalumba | Violet Shivutse | Serah Kiragu-Wissler

SHUKRANI

Kijitabu hiki kinaeleza miongozo ya kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha ya Magharibi. Aidha kinaeleza jinsi jamii ya Isukha ya Magharibi ilivyoandaa utaratibu na miongozo ya kukodisha ardhi. Lengo la kukuza vidokezo vinavyoongoza ukodishaji wa ardhi ya jumuiya lilikuwa kukuza mwafaka wa umiliki wa kukodisha ardhi kwa lengo la kilimo na kuhakikisha mahusiano mema baina ya mkodishaji na mmiliki. Jumuiya pia ilianda fomu ya mkataba wa kukodisha ardhi. Fomu hii imejumuishwa katika kijitabu hiki.

Msukumo wa kuimarisha mwafaka wa umiliki wa ukodishaji ardhi unaambatana na mafunzo yaliyofanyika Kisumu mwezi Februari 2016 katika warsha ya washikadau mbalimbali kutoka vitengo kadhaa. Katika warsha hii, washiriki wote walikubaliana juu ya mambo ya kimsingi yatakayozingatiwa ili kuwezesha usimamizi wa ardhi kiendelevu zaidi Magharibi mwa Kenya.

Mradi huu wa kijumuiya ulifanikishwa kupitia ufadhili kutoka kwa Wizara ya Ujerumani ya Ushirikiano wa Kiuchumi (BMZ) na msaada wa kiufundi kutoka kwa TMG Research gGmbH, Berlin na Wafanyakazi wa Shirika la Afya ya Jamii la Shibuye (Shibuye Community Health Workers/SCHW), Shinyalu (CBO-Community Based Organization).

Shukrani maalum kwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya ya Jamii la Shibuye, Bi Violet Khayecha Shivutse kwa kutoa uongozi kwa ajili ya maandalizi ya miongozo ya kukodisha ardhi. Shukrani kuu pia iwaendee watu wa Isukha ya Magharibi na viongozi wao kwa kuratibu na kuandaa mchakato wa miongozo ya kukodisha ardhi kwa hamu kubwa. Tunaitambua pia Serikali ya Gatuzi la Kakamega (County Government of Kakamega/CGK) kwa kutambua na kusaidia mchakato wa kukuza miongozo ya kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha ya Magharibi.

Doreen Magotsi ni afisa wa programu wa Shirika la Afya la Jamii la Shibuye (SCHW) CBO

William Onura Akwanyi ni mtafiti msaidizi katika Kituo cha Mafunzo na Utafiti Mseto katika Maendeleo ya ASAL (CETRAD)

Linet Khalumba ni afisa msaidizi katika Shirika la Afya ya Jamii la Shibuye (SCHW) CBO, Shinyalu

Violet Shivutse ni mkurugenzi wa Shirika la Afya ya Jamii, Shibuy (SCHW) CBO, Shinyalu

Serah Kiragu-Wissler ni mtafiti katika taasisi ya utafiti, TMG ThinkTank for Sustainability, Berlin

Ukurasa wa juu una picha inayoonyesha: Washiriki katika uzinduzi wa Mwongozo na Mchakato wa kuhamasisha jamii katika kanisa la Munasio PAG katika kata ndogo ya Mukhonje © Violet Shivutse

VIDOKEZO VYA MWONGOZO WA JUMUIYA VYA KUKODISHA ARDHI

**WADI YA ISUKHA YA MAGHARIBI, GATUZI NDOGO LA SHINYALU
KAUNTI YA KAKAMEGA**

Doreen Magotsi | William Onura Akwany | Linet Khalumba | Violet Shivutse | Serah Kiragu-Wissler

YALIYOMO

SHUKRANI i

USULI WA VIDOKEZO VYA KUKODISHA ARDHI: UKODISHAJI WA
ARDHI ILI KUIMARISHA UPATIKANAJI WA SHAMBA LA KILIMO 1

UTARATIBU WA MAANDALIZI YA VIDOKEZO VYA KUKODISHA ARDHI 2

- 1 | Uhamasisho, mashauriano na mazungumzo kati ya washikadau wa taasisi na jamii ya Isukha Magharibi 2
- 2 | Kukusanya watu katika kiwango cha jamii (kamati za kata ndogo) 3
- 3 | Uandishi wa miongozo ya kukodisha ardhi (kamati ya kuaandaa rasimu) 3
- 4 | Kujumuishwa na kudhinishwa kwa miongozo ya kukodisha ardhi 4
- 5 | Uzinduzi wa miongozo wa kukodisha ardhi 5
- 6 | Utekelezaji na ufuatiliaji wa vidokezo vya kukodisha ardhi 6

MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI 7

- 1 | Kamati Jamii ya kukodisha ardhi 7
- 2 | Utaratibu wa kukodisha ardhi 8
- 3 | Masharti 11

FOMU YA MKATABA WA KUKODISHA ARDHI 16

USULI WA VIDOKEZO VYA KUKODISHA ARDHI: UKODISHAJI WA ARDHI ILI KUIMARISHA UPATIKANAJI WA SHAMBA LA KILIMO



Msimamizi wa Wadi akitoa maoni yake katika ufunguzi wa mkutano wa uhamasisho na mashauriano ya miongozo ya ukodishaji wa ardhi katika kanisa la Munasio PAG katika kata ndogo ya Mukhonje © Doreen Magotsi

Kilimo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya kiuchumi nchini Kenya. Ni shughuli kubwa ya kiuchumi kwa jamii nyingi. Njia ya kawaida ya kupata ardhi ya kilimo katika Magharibi mwa Kenya ni kupitia urithi. Kulingana na sheria za kitamaduni za urithi wa ardhi, vipande vya ardhi vya familia viko mikononi mwa wazee wa kiume wa familia na hupokezwa kwa wanao wa kiume wa familia wanapokomaa na kutosha kutunza ardhi. Umiliki wa ardhi ya familia kwa wanawake ni kupitia waume zao na unategemea uhusiano wao na waume zao. Kuongezeka kwa idadi ya watu kumesababisha mgawanyiko wa ardhi kwa kiasi kwamba vipande vidogo havina dhamana kwa kilimo. Vizuizi vya upatikanaji wa ardhi ni kikwazo kikubwa kwa kuendeleza kilimo. Katika hali nyingi, vijana na wanawake hukumbwa na vizuizi vya matumizi ya ardhi.

Katika familia ilio na watu wengi wasio na ardhi kwa kilimo, njia pekee iliyobaki ya wao kupata ardhi hii ni kwa kukodisha.

Ukodishaji wa ardhi vijijini kwa kawaida hufanyika katika vikao visivyoo rasmi kama vile njiani, makanisani au sokoni. Mipango mingine ya kukodisha hufanyika bila kuhusishwa kwa wahusika muhimu kama vile mke na wanafamilia. Katika matukio mengi, hakuna mikataba iliyoandikwa wala mashahidi kwa mipangilio ya kukodisha ardhi. Hali hii inawaweka wahusika katika

hatari kama vile kukatizwa kwa mapema kwa mikataba ya kukodisha, kukodisha kwa muda mrefu usiyopangwa au hata migogoro juu ya kugawana mazao au rasilimali kwenye ardhi iliyokodishwa. Kutokana na migogoro hii, jamii ya wadi ya Isukha Magharibi katika gatuji ndogo la Shinyalu, Gatuji la Kakamega iliamua kuandaa miongozo ya kusimamia mipango ya kukodisha ardhi.

Utaratibu wa kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi ulifanywa na Wafanyakazi wa shirika la afya ya Jamii la Shibuye (Shibuye Community Health Workers/SCHW), shirika la kijamii linalofanya kazi katika Gatuji la Kakamega, kwa msaada wa kiufundi kutoka TMG Research gGmbH, Berlin. Inatarajiwa kuwa miongozo hii itasaidia kutatua migogoro mingi inayohusiana na ukodishaji ardhi.

UTARATIBU WA MAANDALIZI YA VIDOKEZO VYA KUKODISHA ARDHI

Utaratibu huo ulijumuisha hatua zifuatazo:

- 1) Uhamasisho, mashauriano na majadiliano kati ya washikadau wa taasisi za jamii ya wadi ya Isukha ya Magharibi;
 - 2) Ukusanyaji wa watu na mashauriano katika kiwango cha kijamii;
 - 3) Kuandika miongozo ya kukodisha ardhi;
 - 4) Kujumuisha na kuidhinishwa kwa miongozo ya kukodisha ardhi;
 - 5) Uzinduzi wa miongozo ya kukodisha ardhi; na
 - 6) Utekelezaji na ufuatiliaji wa miongozo ya kukodisha ardhi.
- a) Msimamizi wa wadi, Wadi ya Isukha ya Magharibi;
 - b) Afisa wa kilimo, Wadi ya Isukha ya Magharibi;
 - c) Wawakilishi kutoka Bodi ya Kudhibiti Ardhi (Land Control Board/LCB), Gatuzi ndogo la Shinyalu;
 - d) Chifu, Kata ya Ileshi;
 - e) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Mukhonje;
 - f) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Mugomari;
 - g) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Malimili;
 - h) Baadhi ya wazee wa kijiji kutoka Wadi ya Isukha ya Magharibi; na
 - i) Baadhi ya afisa wa *nyumba kumi* (walinzi wa kijiji) kutoka Wadi ya Isukha Magharibi.

1 | UHAMASISHO, MASHAURIANO NA MAJADILIANO KATI YA WASHIKADAU WA TAASISI ZA JAMII YA WADI YA ISUKHA MAGHARIBI

Hatua hii ya kwanza ililenga kueleza dhana ya miongozo ya kukodisha ardhi kwa washikadau wa taasisi na wanajamii katika wadi ya Isukha ya Magharibi kwa lengo la kupata makubaliano na michango yao katika utaratibu huo. Kikao hiki kilifanyika kupitia Baraza (mkutano wa umma) katika Kanisa la Munasio Pentecostal Assemblies of God (PAG) katika kata ndogo ya Mukhonje mnamo tarehe Moja (1) Novemba 2017. Wakati wa mkutano huo, Wafanyakazi wa shirika la Afya ya Jamii la Shibuye walijadiliana na wadau wa jamii na washiriki wa taasisi, juu ya wazo la kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha ya Magharibi na utaratibu wa kuzingatiwa. Washiriki walijumuisha:

Mawazo kuhusu ukodishaji wa ardhi na utaratibu wa kuzingatiwa yalikuwabiwa kwa pamoja baina ya wadau wa taasisi na wanajamii wa mitaa. Mawaazo ya kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha Magharibi yalichukuliwa kama hatua iliyofaa ili kupunguza migogoro inayohusiana na ukodishaji wa ardhi.

Ingawa fomu ya kukodisha ardhi ilisemekana kuwepo kwenye tovuti ya Wizara ya Ardhi, jamii ya eneo hilo haikuwa imewahi kuona wala kuitumia. Mwakilishi kutoka Bodi ya Udhhibiti wa Ardhi (Land Control Board/LCB) aliarifu kikundi cha watu kwamba waliokuwa na nia ya kukodisha ardhi walitarajiwa kuipakua fomu, kujaza na kisha kulipa ada ya KES.1,000 kwa wakili ili iadhiinishwe. Washiriki walihisi kwamba utaratibu wa ukiritimba wa kupata fomu hiyo haukutitia maanani mahitaji yao ambayo ni urahisi wa upatikanaji, kuijaza na, uwezo wa kuelewa utaratibu wa kukodisha ardhi.

2 | KUKUSANYA WATU KATIKA KIWANGO CHA JAMII (KAMATI ZA KATA NDOGO)

Ukusanyaji wa watu ulifanyika mnamo Novemba 2017 kupitia mikutano minne katika kata ndogo. Lengo la mikutano lilikuwa kuwezesha ushiriki wa watu wengi katika wadi katika maandalizi ya miongozo ya kukodisha ardhi. Kila kamati ya kata ndogo ilijumuisha naibu wa chifu, wakuu wa kijiji, baadhi ya viongozi wa nyumba kumi (walinzi wa kijiji), wawakilishi wa Bodi ya Udhhibiti wa Ardhi (Land Control Board/LCB) na viongozi wa jumuiya za mitaa wanaojumuisha wanaume, wanawake na vijana ambao waliwakilisha makundi tofauti katika jumuiya kama vile wakulima wadogo, viongozi wa maoni, maafisa waliostaafu kutoka kwa huduma ya umma, viongozi wa kanisa, wajane, wakodishaji na wamiliki. Mikutano hii ya kamati iliongozwa na naibu wa chifu wa eneo husika. Chifu wa eneo hilo, msimamizi wa kata ndogo na wawakilishi kutoka Bodi ya Udhhibiti wa Ardhi (Land Control Board/LCB) walihudhuria mikutano ya kamati ndogo na ya kuandaa rasimu.

Kamati nne za kata ndogo zilihusisha Mukhonje A, Mukhonje B, Malimili na Mugomari. Kila kamati ilikuwa na takribani watu thelathini (30). Kata ndogo ya Mukhonje liligawanywa katika kamati mbili kutokana na ukubwa wake.

Mipango wa kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi ilikubalika katika maeneo yote ya wadi ndogo. Mshiriki kutoka kata ndogo ya Malimili alikuwa na furaha sana kuhusiana na wazo hili na alikuwa na haya ya kusema:

“Mimi ni mzee katika jamii hii na ninafurahia mpango huu wa kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi. Kwa miaka mingi niliyoishi hapa, sijawahi kushuhudia mradi kama huu. Pia ninafurahia sana kuwa, watu wengi wamelikumbatia wazo hili.”

Kulikuwa na maoni tofauti ya masuala ya kuzingatiwa kuhusiana na miongozo ya kukodisha ardhi kutoka kwa kamati hizi. Baadhi ya masuala ambayo yalijadiliwa katika kamati hizi ni pamoja na: utaratibu wa kukodisha ardhi; uthibitishaji wa mipaka ya ardhi na umiliki; uthibitisho wa ukosefu wa vizuizi kwenye ardhi; utambulisho na ushiriki wa wanafamilia na mashahidi; muda wa kukodisha; kukatisha kwa mkataba wa kukodisha; kamati ya kukodisha ardhi; masharti ya kukodisha na fomu ya mkataba ya kukodisha ardhi. Kileleni mwa uhamasishaji na utambuzi wa masuala muhimu yaliyopaswa kuzingatiwa katika ukukodisha wa ardhi, kamati za kata ndogo zilichagua kamati za kuandaa rasimu ambazo zingejadili masuala haya kwa upana zaidi.

3 | UANDISHI WA MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI (KAMATI ZA KUANDAA RASIMU)

Lengo la kamati za kuandaa rasimu lilikuwa ni kuzingatia masuala yaliyoibuliwa katika kamati za kata ndogo za kuandika miongozo ya kukodisha ardhi. Kulikuwa na kamati (3) za kuandika rasimu, kila moja ya kamati ya kuandika rasimu iliwakilishwa na watu wapatao kumi na watano (15) na ilifanya vikao visivyo chini ya vitatu (3) kwa siku tatu (3). Mukhonje A ilichagua watu 8 na Mukhonje B ilichagua watu saba (7). Kwa pamoja walikuwa watu kumi na watano (15) katika kamati ya kuandika rasimu ya kata ndogo ya Mukhonje.



Mkutano wa ujumuishaji wa miongozo ya kukodisha ardhi katika kanisa la Munasio PAG katika kata ndogo ya Mukhonje © William Onura

4 | KUJUMUISHWA NA KUIDHINISHWA KWA MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI

Rasimu za miongozo ya kukodisha ardhi na fomu ya mkataba ya kukodisha ardhi kutoka kwa kamati za kuandaa rasimu ilijadiliwa na Kujumuishwa kama mwongozo wa kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha ya Magharibi katika mkutano uliofanyika tarehe 21 Novemba, 2017 katika Kanisa la Munasio Pentecostal Assemblies of God (P.A.G.). Lengo la mkutano lilikuwa kuleta makubaliano juu ya masuala na mapendekezo yaliyoandaliwa na kamati za kuandaa rasimu za miongozo ya kukodisha ardhi.

Mkutano ulijumuisha watu arobaini (40) wakiwemo wafuatao:

- a) Msimamizi wa wadi, Wadi ya Isukha ya Magharibi;
- b) Afisa wa kilimo, Wadi ya Isukha ya Magharibi;
- c) Wawakilishi kutoka Bodi ya Kudhibiti Ardhi (LCB), Gatuzi ndogo la Shinyalu;
- d) Chifu, Kata ya Ileshi;
- e) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Mukhonje;
- f) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Mugomari;
- g) Naibu wa Chifu, Kata ndogo ya Malimili;
- h) Baadhi ya wazee wa kijiji kutoka wadi ya Isukha ya Magharibi;
- i) Baadhi ya maafisa wa *nyumba kumi* (walinzi wa kijiji) kutoka wadi ya Isukha Magharibi; na
- j) Wajumbe waliochaguliwa katika kamati za kuandaa rasimu kutoka kwa sehemu zote za kata ndogo.

Kamati ya ujumuishaji iliweka pamoja Mwongozo wa kukodisha ardhi na Fomu ya mkataba wa kukodisha ardhi ya wadi ya Isukha ya Magharibi.

5 | UZINDUZI WA MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI

Hatua hii ilinua kuzindua miongozo na kujenga uhamasisho wa kuwepo kwake katika kiwango cha kata ndogo. Mkutano wa uzinduzi ulifanyika Ijumaa tarehe 12 Januari 2018 katika kanisa la Munasio PAG. Mkutano ulihudhuriwa na wanachama wote wa kamati za kuandaa rasimu pamoja na viongozi wa jamii ambao walikuwapa katika kamati za ujumuishaji.

Wanajamii ya Isukha Magharibi waliwashukuru wafanyakazi wa shirika la Afya ya Jamii la Shibuye kwa kuhakikisha uhusika na ushiriki wa watu katika wadi nzima. Washiriki walikuwa na matumaini kwamba miongozo ya kukodisha ardhi ingesaidia kuzuia migogoro kuhusiana na ukodishaji wa ardhi.

Yafuatayo ni baadhi ya maoni kutoka kwa washiriki wawili:

“Ninafuraha sana na wazo la kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi. Watu wengi katika eneo hili wameteseka chini ya mikono ya wamiliki na wakodishaji walafi. Natumaini kwamba hatutakuwa na watu wanaodhulumiwa na wamiliki na wakodishaji hawa walafi kama miongozo hii itatekelezwa kwa njia sahihi.” Everline Malieto

“Tunafurahi kuwa sasa tumepata suluhisho la migogoro kuhusiana na kukodisha ardhi ambayo ni kawaida katika eneo hili. Kwa kweli ikiwa sisi wote tunakubali miongozo hii na kuwa mabalozi wa miongozo hii kwa wajumbe wengine wa jamii, basi sisi kama viongozi tutakuwa na muda mwingi wa kushughulikia majukumu mengine badala ya migogoro inayohusiana na ardhi.” Chifu Mwandamizi, kata ya Ilesi

“Ninawapongeza watu wa wadi ya Isukha Magharibi kwa kuandaa miongozo ya kukodisha ardhi. Kwa ruhusa yenu nitatumia miongozo hii katika eneo langu la kuzaliwa la Lugari.” Msimamizi wa Wadi ya Isukha Magharibi



Washiriki katika mkutano wa uzinduzi katika kanisa la Munasio PAG katika kata ndogo ya Mukhonje © William Onura

Jamii ilisisitiza haja ya kueneza miongozo ya kukodisha ardhi ili kila mtu katika vijiji atambue kuwepo kwake na aweze kutumia.

6 | UTEKELEZAJI NA UFUATILIAJI WA MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI

Fomu ya mkataba ya kukodisha ardhi ya wadi ya Isukha Magharibi itawasilishwa kwa ajili ya matumizi ya kila mtu anayejihusisha na shughuli za kukodisha ardhi katika wadi ya Isukha Magharibi. Fomu hii itapatikana katika afisi za Naibu wa Chifu, afisi za Chifu na afisi za Shirika la Afya ya Jamii la Shibuye-Shinyalu. Jumuiya ya mitaa inapendekeza kuundwa kwa Kamati ya Kukodisha Ardhi ya Jumuiya, itakayoongozwa na Naibu wa Chifu katika eneo lake. Kamati hii itasimamia utekelezaji wa utaratibu wa kukodisha ardhi. Wajumbe wengine wa kamati watakuwa Chifu wa eneo, mzee wa kijiji, mwakilishi

wa wanaume, mwakilishi wa vijana ambaye pia ni mkulima, mwakilishi wa Bodi ya Udhhibiti wa Ardhi (LCB), Msimamizi wa Wadi, mwakilishi kutoka kwa kundi la kiraia na mshauri wa kiufundi kutoka afisi za kilimo. Kamati itakutana mara kwa mara ili kuchunguza utekelezaji wa miongozo ya kukodisha ardhi na kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya watumiaji. Kamati pia itaimarisha masuala yanayojitokeza ambayo yanaweza kuhitaji marekebisho ya miongozo ya kukodisha ardhi.

Utaratibu wa kuandaa Mwongozo wa Kukodisha Ardhi umewasilishwa katika kielelezo kifuatacho:

Jedwali 1: Mchakato wa kuandaa Mwongozo wa Jumuiya wa Kukodisha Ardhi (CL-LLG)



MIONGOZO YA KUKODISHA ARDHI

Ifuatayo ni Miongozo ya Kukodisha Ardhi kama ilivyotengenezwa na Jamii ya eneo la Isukha ya Magharibi baina ya Mwezi wa Oktoba 2017 na Januari 2018.

1 | KAMATI YA JAMII YA KUKODISHA ARDHI

Kamati ya kusimamia shughuli za kukodisha ardhi itaanzishwa katika wadi ya Isukha Magharibi. Kamati hii aidha itaanzishwa katika kila kata ndogo. Kamati hiyo itajulikana kama Kamati ya jamii ya kukodisha Ardhi. Kamati itakuwa na wanakamati wafuatao:

- a) Msimamizi wa wadi - ambaye atakuwa mwanachama asiye rasmi wa kamati
- b) Chifu wa eneo - ambaye atakuwa mwanachama asiye rasmi wa kamati
- c) Naibu wa chifu - ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati
- d) Mwakilishi mmoja wa Shirika la Kiraia (Civil Society Organizations-CSOs) - ambaye atakuwa katibu katika mikutano yote ya kamati
- e) Mwakilishi mmoja kutoka Bodi ya Udhhibiti wa Ardhi (Land Control Board-LCB) - atatoa ushauri wa kiufundi kwa kamati
- f) Afisa wa kilimo wa kata - atatoa ushauri wa kiufundi kwa kamati
- g) Mwakilishi mmoja wa wazee wa kijiji - mapendeleo yatapewa mzee mwandamizi wa kijiji

h) Mwakilishi mmoja wa vijana - lazima awe mkulima na mwenye umri kati ya miaka 18 na 35

i) Mwakilishi mmoja wa wanawake - atatoka makundi yote ya wanawake ikiwa ni pamoja na walio katika ndoa, waliopewa talaka, waliotengana na waume na wajane

j) Mwakilishi mmoja wa wanaume - atachaguliwa tu pale ambapo zaidi ya nusu ya wanachama wa kamati watakuwa ni wanawake

Kamati itakuwa na wanachama wasiozidi tisa (9) wakati wowote. Idadi hii haijumuishi wanachama wasio rasmi. Wawakilishi wa wazee wa kijiji, vijana, wanawake na wanaume wanaohitajika watateuliwa au kuchaguliwa kutoka kwa jumuiya wakati wa *Baraza* (mkutano wa umma). Utaratibu wa uteuzi au uchaguzi wa wanachama wa kamati ya kukodisha ardhi ya jamii utafanyika hadharani na utahusisha ushiriki wa watu wote katika jamii katika mkutano wa baraza.

Kamati itachagua mweka hazina. Wanachama wasio-rasmi, naibu wa chifu (kama mwenyekiti) na mwakilishi wa asasi za kiraia (Civil Society Organizations-CSOs-kama katibu) hawatatahili kuchaguliwa katika nafasi ya mweka hazina. Mweka hazina atakuwa na jukumu la kuweka fedha zilizokusanywa kutokana na faini au fedha zozote zinazohusiana na shughuli za kukodisha ardhi. Fedha zitatumiwa kuwezesha mikutano ya kamati na madhumuni mengine kama itakavyoamuliwa na kamati.

Kamati itakuwa na mikutano katika kila robo ya mwaka kujadili masuala yanayohusiana na kukodisha ardhi katika maeneo ya kata ndogo. Kamati inaweza kuwa na kikao maalum kulingana na kesi au dharura inayohitaji mikutano hiyo.

Naibu wa Chifu atakuwa mtunzaji na mhifadhi wa sajili za shughuli zote za kukodisha ardhi katika kata-ndogo yake na ataeleza kamati juu ya shughuli zote za kukodisha ardhi katika kata ndogo yake ili kukagua na kutathmini utekelezaji wa miongozo ya kukodisha ardhi.

Majukumu ya kamati yatakuwa:

- 1) Kusimamia shughuli za kukodisha ardhi katika ngazi ya kata ndogo.
- 2) Kuchunguza masuala ibuka yanayojitokeza na yanaweza kuhitaji marekebisho ya miongozo ya kukodisha ardhi.
- 3) Kutatua migogoro inayohusiana na kukodisha ardhi. Kamati inaweza wakati wa mkutano wake kuwaalika wahusika walioathirika na migogoro ya kukodisha ardhi.

2 | UTARATIBU WA KUKODISHA ARDHI

- 1) Mkodishaji (mtu mwenye nia ya kukodisha ardhi) kabla ya kukodisha sehemu yoyote ya ardhi atahitaji:
 - a) Kutambua kipande cha ardhi anachotaka kukodisha.
 - b) Kutambua mmiliki wa ardhi ambayo anataka kukodisha.
 - c) Kuwashirikisha jamaa au ndugu zake hasa mke na watoto au marafiki wa karibu na iwezekanapo jamaa wa karibu katika eneo ambalo anataka kukodisha ardhi. Hivyo basi, jamaa wa karibu huyu lazima atajulishwa.

d) Hakikisha kwamba familia za mmiliki wa ardhi zinahusishwa ili kupunguza migogoro.

e) Thibitisha kuwa kipande cha ardhi ambacho unataka kukodisha ni cha mmiliki kwa kuomba moja au zaidi ya hati zifuatazo:

i) Hati miliki ya ardhi

ii) Hati ya kukodisha

iii) Barua ya ugawaji

iv) Hati kiapo

v) Cheti cha utafutaji rasmi kutoka kwa afisi ya msajili wa ardhi

vi) Hati yoyote au ushahidi ulioidhinishwa na sheria za Kenya au kamati ya kukodisha ardhi

f) Thibitisha maelezo ya nyaraka zilizotajwa kwa kuzingatia utambulisho wa mmiliki wa ardhi kama vile kitambulisho cha kitaifa au pasipoti halali ya Kenya.

g) Iwapo hakuna nyaraka za kuthibitisha umiliki au iwapo nyaraka hizi ni za gharama kubwa kupatikana, uthibiti wa umiliki wa ardhi unaweza kupatikana kutoka kwa familia ya mmiliki au kutoka kwa majirani au wazee na viongozi wa eneo ambalo ardhi ya kukodishwa inapatikana. Hii ni kwa sababu wanafamilia hawa, majirani, wazee na viongozi wamekuwa wakazi katika eneo hilo kwa muda mrefu na hivyo kuelewa masuala ya umiliki wa ardhi katika eneo hilo.

h) Kuthibitisha kwamba kipande cha ardhi anachotaka kukodisha hakina migogoro (bila vikwazo) kwa kushauriana na wanafamilia, majirani, wazee, viongozi wa mitaa, wakodishaji wa zamani wa ardhi hiyo na kamati ya kukodisha ardhi.

-
- i) Kuhakikisha mkataba wa kukodisha ardhi umeandikwa vizuri, umetiwa sahihi na umeidhinishwa na yeye pamoja na mmiliki wa ardhi mbele ya mzee wa kijiji na naibu wa Chifu wa eneo au Chifu wa eneo ambalo sehemu ya ardhi ya kukodisha inapatikana.
 - 2) Mmiliki (mmiliki wa ardhi) kabla ya kukodisha sehemu yoyote ya ardhi atahitaji:
 - a) Kushirikisha jamaa wa familia au marafiki wa karibu.
 - b) Hakikisha kuwa familia au jamaa wa mkodishaji hasa mke na watoto wanahusika ili kupunguza mizozo ya kifamilia.
 - c) Kumpa mkodishaji idhini ya kutosha kwa kipande cha ardhi kilichokodishwa.
 - d) Kuwapa majirani njia ya kufikia mali au vitu vyao kama vile nyumba au ardhi inayopatikana nyuma ya ardhi iliyokodishwa.
 - e) Ruhusu ufikiaji wa vitu na rasilimali za umma kama vile visima vya maji na chemchemi zilizohifadhiwa ambazo ziko ndani ya ardhi iliyokodishwa.
 - f) Washauri wapangaji kuhusu sehemu au waliofanya maendeleo yoyote katika ardhi ya kukodisha ambayo haipaswi kuingiliwa.
 - g) Toa maelezo sahihi juu yake na hali ya ardhi ambayo yeye anataka kukodisha.
 - h) Hakikisha mkataba wa kukodisha umeandikwa vizuri na umetiwa sahihi na kuidhinishwa na mmiliki pamoja na mkodishaji mbele ya mzee wa kijiji na Naibu wa Chifu au Chifu wa eneo ambalo ardhi ya kukodishwa inapatikana.
 - 3) Mkodishaji na mmiliki watazingatia yafuatayo katika mchakato na shughuli zinazohusiana na kukodisha ardhi:
 - a) Shirikisha kamati ya kukodisha ardhi ya jamii na kusajili mkataba na kamati hii.
 - b) Wasiingie makubaliano ya kukodisha ardhi ya serikali, hifadhi za barabara, ardhi ya watu wengine au taasisi au ardhi ambayo inahifadhiwa chini ya sheria kama maeneo ya mito (maeneo yaliyo kwenye mabonde na mito).
 - c) Wakubaliane kuhusiana na aina ya ukukodishaji (muda mfupi au mrefu) ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kuwepo kwa mkataba upya.
 - d) Wakubaliane juu ya ukubwa wa ardhi ya kukodishwa na mipaka yake, kwa kutoa maelezo ya wazi, watumie alama muhimu kwenye ardhi hiyo kama miti, barabara, matuta, majengo, mito, miamba na makaburi kati ya mengineyo. Ramani ya mchoro inaweza kuchorwa kwa kutumia vipengele hivi. Ikiwa ramani ya eneo inapatikana inaweza kujumuishwa.
 - e) Wakubaliane juu ya haki za kumiliki na matumizi ya ardhi, na kiwango cha uhuru wa mkodishaji na uhibitaji wa mmiliki wa ardhi iliyokodishwa pamoja na:
 - i) Matumizi yaliyokusudiwa ikiwa ni pamoja na majina ya mimea ya kupandwa, idadi ya matofali ya kutengenezwa na kiasi cha dhahabu cha kuchimbwa au udongo utakaotolewa - awapo matumizi ya ardhi yanalenga madhumuni mengine yasiyo kilimo.
 - ii) Mipango ya ukaguzi wa ardhi iliyokodishwa na mmiliki wa ardhi.

- iii) Fursa kwa mwenyeji kutumia mali nyingine au miundombinu kwenye ardhi iliyokodishwa kama vile mimea ya kudumu ikiwa ni pamoja na miti ya matunda na chakula; vyoo vya shimo; na sehemu za maji ikiwa ni pamoja na tanki la kuvuna maji, visima, mabwawa na chemchemi kati ya mengine.
 - iv) Jukumu la wa kulinda kipande cha ardhi kilichokodishwa kwa kutia ua na kuboresha kiwango chake cha rotuba kupitia njia endelevu za udhibiti wa ardhi kama vile kuweka chokaa, kutengeneza mitaro, kuweka mbolea na kupanda miti.
 - v) Uwajibikaji katika kudumisha miundombinu kama barabara, ua, matuta, vidimbwi vya maji; na rasimali kama vile miti na mimea ya lishe ya mifugo.
 - vi) Uwezekano wa mmiliki wa ardhi kupata na kutumia miundombinu kama vile vyoo vya shimo na vidimbwi vya maji; mali kama vile miti na mimea ya lishe ya mifugo; na maeneo ya kitamaduni kama vile mahali patakatifu/madhabahu na makaburi.
- f) Wakubaliane kuhusu kipindi cha kukodisha ikiwa ni pamoja na muda wa kukodisha, wakati gani eneo la kukodisha litakabiliwa mkodishaji na litakaporejeshewa mmiliki wa ardhi. Wakati mwingine watu wanaruhusu wengine kutumia ardhi yao mpaka wakati ambapo watoto wa mmiliki watakuwa wamekomaa na kuwa na uwezo wa kutumia ardhi hiyo. Katika muktadha huu umri wa watoto wa mmiliki wa ardhi utatumiwa kama muda wa makubaliano ambapo ardhi itawasilishwa tena kwa mmiliki wa ardhi, umri wa mtoto maalum utazingatiwa.
- g) Wakubaliana juu ya urahisishaji wa kukodesha ikiwa ni pamoja na marejeleo ya mkataba wa kukodisha na tarehe ya kurejelewa.
- h) Tathmini ya hali ya ardhi wakati mmiliki atarejeshewa ardhi yake mwishoni mwa kipindi cha kukodisha: Hali ya ardhi itaelezwa kwa maandishi kabla ya kupewa mmiliki. Hali hii itatoa msingi wa kuamua hali inayohitajika wakati ardhi itarejeshewa mmiliki mwishoni wa kipindi cha kukodisha ikiwa ni pamoja na kuhifadhi miundo msingi kama vile ua, mifereji na tanki za kuvuna maji na matuta.
- i) Weka viwango vya fidia au ada itakayotolewa kutokana na kukodisha ardhi. Hii inaweza kuwa pesa ya kulipwa, sehemu ya mavuno ya mimea, au sehemu ya bidhaa nyingine kutoka kwenye shamba kama vile visiki vilivyofukuliwa kwenye shamba kwa matumizi ya kuni au mawe yaliyotibuliwa kutoka kwenye kipande cha ardhi. Ikiwa ardhi inakodishwa kwa madhumuni mengine badala ya kilimo makubaliano yanaweza kuweka iwapo mmiliki na mkodishaji watagawana madini kutoka kwenye ardhi kama vile dhahabu; au matofali yanayotokana na udongo.
- j) Wakubaliane namna ya kufidia au jinsi ada itakavyoafikiwa, njia ya malipo na adhabu itakayotolewa kwa mkodishaji iwapo atakosa kuhesimu mkataba wa malipo na masharti yaliyokubaliwa.
- k) Wakubaliane juu ya majukumu ya kila mwanachama kuhusu utunzaji wa mimea kwenye ardhi iliyokodishwa.
- l) Waelewe hatari zinazohusika na jinsi ya kuzidhibiti ili kuzuia migogoro. Katika hali hii, mmiliki na mkodishaji watahitajika:

- i) Kuwashirikisha jamaa wa familia zao;
- ii) Kukubaliana na kutambua utaratibu wa kutatua migogoro;
- iii) Kutambua na kuhusisha mashahidi wao ambao wana akili timamu na umri uliokomaa;
- iv) Kukubaliana kwa maandishi hatua na adhabu zitakazochukuliwa ikiwa mkodishaji atatumia ardhi iliyokodishwa vibaya au atakataa kuondoka kwenye ardhi iliyokodishwa mwisho wa kipindi cha kukodisha au kukataa kutii mkataba mwingine wowote;
- v) Kukubaliana kwa maandishi juu ya hatua zitakazochukuliwa ikiwa mmiliki wa ardhi atasitisha mapema mkataba wa kukodisha na kuingilia mimea ya mkodishaji au kuingilia kipande cha ardhi kilichokodishwa katika kipindi ambacho kingali mikononi mwa mkodishaji au uvunjaji wa mkataba wowote na mmiliki wa ardhi;
- vi) Kubaliana kwa maandishi juu ya majukumu yao kwa ardhi iliyokodishwa wakati wa kipindi cha ukodishaji na hatua zitakazochukuliwa iwapo mkataba utavunjwa na pande yoyote; na
- vii) Kubaliana kwa maandishi juu ya fidia au adhabu kwa upande wowote ikiwa kuna uvunjaji wa mkataba.

3 | MASHARTI

1) Umri wa juu: Mtu yeyote mwenye umri wa miaka zaidi ya miaka kumi na nane (18) anaweza kukodisha au kukodishwa ardhi. Mmiliki na mkodishaji lazima wahakikishe kwamba mashahidi wao ni watu wa akili

timamu na wana umri wa miaka (18). Katika hali ambayo wahusika wako chini ya umri (chini ya miaka 18) au ni yatima au walioachiwa mamlaka ya kuitunza ardhi ya familia ambayo wanataka kuikodisha, naibu wa chifu au chifu watathibitisha kuwa wana mahitaji ya kweli kukodisha ardhi hiyo na wana wawakilishi waliokomaa kiumri na wana akili timamu na afya nzuri kutoka kwa familia zao, jirani au familia zao wanaowachagua ambao wanaweza kuwasimamia kama walezi. Taarifa kuhusu huyu mwakilishi wa watu wazima lazima ieleweke na iambatanishwe na makubaliano ya kukodisha.

- 2) Uhusika wa kamati ya kukodisha ardhi ya jumuiya na usajili wa mkataba wa kukodisha
 - a) Kamati ya kukodisha ardhi ya jumuiya itahusishwa kutoka mwanzo wa utaratibu na kupitia hatua zote.
 - b) Mmiliki na mkodishaji wa ardhi pamoja na mashahidi wao watajaza fomu ya mkataba wa kukodisha ardhi mbele ya naibu wa Chifu au mzee wa kijiji.
 - c) Fomu ya mkataba wa kukodisha ardhi itajazwa na wahusika wote na kutiwa sahihi kwa utatu.
 - d) Naibu wa Chifu au Chifu ataidhinisha fomu zote tatu za mkataba wa kukodisha zilizotiwa sahihi kwenye kurasa zote.
 - e) Naibu wa Chifu au Chifu atasajili rasmi mkataba wa kukodisha.
 - f) Mmiliki wa ardhi, mkodishaji na naibu wa Chifu au Chifu atahifadhi mojawapo ya fomu ya mkataba wa kukodisha ardhi iliyoidhinishwa
 - g) Naibu wa chifu au chifu ataarifu kamati juu ya ardhi iliyokodishwa.

3) Muda wa kukodisha ardhi

Mwaka wa kukodisha ardhi utanza Januari na kumalizika Desemba ya mwaka huo au miaka itakayofuata. Hata hivyo, sababu za kuwepo kwa muda wowote wa kukodisha au mwisho wa kukodisha lazima ziwekwe wazi katika mkataba wa kukodisha. Kipindi cha kukodisha ardhi kitatambuliwa na:

a) Aina ya mimea: muda mfupi ya kukodisha ardhi haipaswi kuzidi mwaka moja (1) wa miezi kumi na miwili (12) ya kalenda ilihali muda mrefu haupaswi kuwa zaidi ya miaka sita (6) ya miezi sabini na miwili (72) ya kalenda. Hata hivyo, kupitia makubaliano, mkataba mpya wa kukodisha wa muda mrefu au mfupi unaweza kuandikwa pindi tu ule wa kwanza unapokamilika.

b) Matumizi ya ardhi: Kukodisha ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo kutategemea aina ya mimea itakayokuzwa. Kukodisha kwa muda mfupi kutatumika kwa madhumuni ya mimea ya kila mwaka ambayo inapandwa katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na mahindi, maharagwe, maharagwe ya soya, mbaazi, mboga, mimea ya nduma, njugu karanga, njugu za bamba na mimea mingine ambayo itapandwa baadaye katika eneo hilo. Kukodisha kwa muda mrefu kutatumika kwa mimea ya kudumu kama vile majani chai yaliyopandwa tayari, miwa, ndizi na mimea mingine mipya ambayo inaweza kupandwa baadaye katika eneo hilo; na matumizi mengine ambayo si ya kilimo kama vile uchimbaji wa madini ya dhahabu, kupanda miti, utengenezaji matofali, uchimbaji wa mchanga wa ufinyanzi, uchimbaji wa changarawe, na nafasi ya biashara; au kama yalivyo makubaliano kati ya mkodishaji na mmiliki wa ardhi.

4) Matumizi ya ardhi

a) Kabla ya kuingia katika makubaliano ya kukodisha ardhi, mmiliki wa ardhi ataelezea waziwazi kwa mkodishaji, maeneo au ardhi ambayo haipaswi kuingiliwa, kama vile, miti, majengo, mahali patakatifu, madhehebu, makaburi.

b) Mkodishaji hawezi kufanya shughuli nyinginezo zozote kwenye ardhi iliyokodishwa kinyume na yale yalioandikwa kwenye mkataba.

c) Katika kukodisha ardhi kwa malengo ya kilimo, mkodishaji atatumia mbinu bora za kilimo.

d) Iwapo ardhi itakodishwa kwa madhumuni mengine isipokuwa yale ya kilimo, sheria za mazingira na zingine husika zitahitajika kuzingatiwa.

e) Iwapo pana tukio la kuingiliwa au shughuli yoyote ya uharibifu au wizi wa mazao kwenye ardhi iliyokodishwa na mkodishaji au mmiliki, sheria inapaswa kuruhusiwa kuchukua mkondo wake.

f) Mmiliki au mkodishaji wa ardhi watajulisha angalau jirani mmoja kuhusu ardhi ya kukodishwa, nia ya kukodisha ardhi na matumizi yaliyopangwa.

g) Matumizi yoyote ya ardhi iliyokodishwa itakayohusu uchimbaji wa rasilimali za asili ndani yake au kwa shughuli ambayo inaweza kusababisha uharibifu wa mazingira, patahitajika kuwepo kwa utathmini wa mazingira na uidhinishaji kutoka kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (National Environment Management Authority-NEMA) kwa mujibu wa sheria za Kenya¹.

¹ Sehemu ya 58 ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Ushauri (EMCA), 1999 (Cap. 387), marekebisho 2015

h) Matumizi yoyote ya ardhi iliyokodishwa kwa njia ambayo itaharibu mazingira itahitaji kwamba mkodishaji kurekebisha ardhi na mazingira yaliyoharibika kwa mujibu wa sheria za Kenya².

5) Majukumu

a) Mmiliki atahitaji:

- i) Kutoingilia mimea au shughuli za mkodishaji kwenye kipande cha ardhi kilichokodishwa;
- ii) kuhakikisha kuwa jamaa zake, marafiki au mifugo hawaingilii mimea au shughuli za mkodishaji kwenye ardhi iliyokodishwa; na
- iii) Kuzingatia mkataba wa kukodisha.

b) Mkodishaji atahitaji:

- i) Kutofanya shughuli nyingine yoyote kwenye ardhi iliyokodishwa isipokuwa ile ambayo pande zote mbili zimekubaliana katika mkataba wa kukodisha;
- ii) Kuhakikisha ulinzi wa mimea yake na shughuli kwenye ardhi iliyokodishwa; na
- iii) Kuzingatia mkataba wa kukodisha.

6) Mashahidi

Mashahidi lazima wawasilishe nyaraka zao za utambulisho kabla ya kukubaliwa kuwa mashahidi juu ya fomu ya mkataba wa kukodisha. Familia zote mbili (jamaa wa karibu na wa mbali) na wasio wa familia wanaweza kutumika kama mashahidi. Kwa ujumla, watu wafuatao wanaweza kutumika kama mashahidi:

- a) Mke/wake au mme/waume.
- b) Mmoja wa watoto au zaidi aliye na umri wa zaidi ya miaka kumi na nane (18), ambapo mmiliki au mkodishaji ana watoto bila kujali ikiwa watoto walizaliwa ndani au nje ya ndoa.
- c) Mzazi mmoja au wote wawili au mlezi.
- d) Ndugu wa mmiliki au mkodishaji.
- e) Rafiki au mwandani.
- f) Ndugu yeyote wa familia.
- g) Jirani wa kipande/sehemu ya ardhi iliyokodishwa.
- h) Mzee wa kijiji katika kijiji ambacho ardhi itakodishwa.

7) Mrithi

Mkodishaji atachagua mrithi wa kipande cha ardhi kilichokodishwa. Huyu anaweza kuwa jamaa wa familia wa karibu au wa mbali.

- 8) Marejeleo ya mkataba wa kukodisha yatakubaliwa baina ya mmiliki na mkodishaji na yatawasilishwa kwa kamati ya kukodisha ardhi. Marejeleo haya yatajumuisha moja au zaidi ya hatua zifuatazo:
 - a) Mabadiliko ya mashahidi;
 - b) Mabadiliko ya matumizi kwenye ardhi iliyokodishwa;
 - c) Marekebisho kwa muda wa kukodisha;
 - d) Kugeuza mipaka ya ardhi iliyokodishwa;
 - e) Mabadiliko katika hali au masharti ya malipo ya udhamini na ada;
 - f) Kupanua au kupunguza kwa eneo la ardhi iliyokodishwa;
 - g) Kuongezeka au kupunguza udhamini na ada zinazotolewa kwa ajili ya kukodisha;

² Sehemu 3(d) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Ushauri (EMCA), 1999 (Cap. 387), marekebisho 2015

h) Mabadiliko katika kiwango cha uhuru na udhibiti wa ardhi baina ya mmiliki na mkodishaji; na

i) Mabadiliko mengine yoyote yale yaliyoandikwa katika fomu ya mkataba wa kukodisha.

9) Ada ya kukodisha

a) Ada ya kukodisha ardhi itategemea aina na ubora wa kipande cha ardhi ambacho kitakodishwa na matumizi yaliyopangwa.

b) Jamii inapendekeza kuwa ada ya chini ya kukodisha kwa muda mfupi itakuwa shilingi taslimu za Kenya elfu nne na mia tano (Kshs. 4,500.00) kwa ekari kwa mwaka na kiwango cha juu cha shilingi taslimu za Kenya elfu kumi na tano (Kshs. 15,000.00) kwa ekari kwa mwaka kwa ukodishaji wa muda mfrefu.

c) Kiwango cha ada cha kukodisha majani chai kitakuwa kwa mujibu wa mfumo wa Mamlaka ya Maendeleo ya Chai ya Kenya (Kenya Tea Development Authority-KTDA).

d) Kiwango cha ada cha matumizi ya ardhi kwa madhumuni mengine isipokuwa kilimo kitazingatiwa kwa kuzingatia moja au zaidi ya mambo yafuatayo lakini hayatabaki haya tu: kama idadi ya matofali yaliyotengenezwa, malori ya maramu na kiasi cha dhahabu au udongo; kiwango cha uchimbaji; ekari; na wakati.

e) Takwimu ambazo zimeorodheshwa katika (b) hapo juu ni takwimu zinazoongoza ambapo sababu zingine kama vile uhusiano kati ya mmiliki wa ardhi na mkodishaji unaweza kuzingatia na kwa hivyo uamuzi wa mwisho wa ada ya kukodisha utategemea uhusiano baina ya mmiliki na mkodishaji.

10) Ukamilikaji wa mkataba

Mkataba unaweza kuvunjwa unapokamilika au pale ambapo mmiliki na mkodishaji wa ardhi hukubaliana kufanya hivyo kulingana na sababu zao wenyewe na masharti na kujiwasilisha kwa kamati ya kukodisha ardhi ya jamii ili kuvunja makubaliano ya kukodisha.

11) Kuvunjika kwa mkataba

a) Kuvunjaji wa mkataba kutahusisha moja au zaidi ya yafuatayo:

i) Ikingunduliwa kuwa mkodishaji anakuziwa mimea haramu kama vile bangi kwenye ardhi iliyokodishwa;

ii) Kushindwa kwa mkodishaji kulipa ada waliyokubaliana kwa muda ufaao;

iii) Mmiliki anapoharibu mimea au mali au kuingilia katika shughuli za mkodishaji wa ardhi iliyokodishwa;

iv) Mkodishaji anapoharibu kipande cha ardhi kilichokodishwa au mazingira mengine zaidi ya viwango vilivyowekwa katika mkataba wa kukodisha;

v) Mmiliki asipoziua familia, mifugo au marafiki zake kuharibu mimea au mali au kuingiliana shughuli za mkodishaji katika ardhi iliyokodishwa; na

vi) Kushindwa kwa mmiliki au mkodishaji kuzingatia masharti yaliyowekwa katika mkataba wa kukodisha

b) Kutokana na sababu zozote zitakazosababisha upande wowote kuvunja mkataba, adhabu ya hadi asilimia mia moja (100 %) ya ada ya awali waliyokubaliana pamoja na fidia sawa na thamani ya mimea iliyoharibiwa kulingana na miongozo ya Kilimo juu ya uharibifu wa mimea au shughuli zitakazosababisha uharibifu wa ardhi kama itakavyoshauriwa na kamati ya kukodisha ardhi au afisi nyingine yoyote ya kisheria, aliye na hatia atalipa mbele ya kamati ya kukodisha ardhi ya jamii au mwakilishi wake.



Washiriki katika mkutano wa uzinduzi katika kanisa la PG katika kata ndogo ya Mukhonje © William Onura

**FOMU YA MKATABA WA KUKODISHA ARDHI
WADI YA ISUKHA-MAGHARIBI
(Ijazwe katika utatu)**

Fomu hii ya Mkataba wa Kukodisha Ardhi ilitayarishwa mwaka wa 2017 na Jamii za Wadi ya Isukha-Magharibi kwa msaada kutoka kwa wafanyakazi wa Shirika la Afya ya Jamii la Shibuye (CBO) na inalenga kuwezesha mahusiano mema katika kukodisha ardhi.

1. Siku ya Mkataba: (Siku/Mwezi/Maka) _____

2. Wahusika katika Mkataba

Maelezo juu ya Mmiliki		Maelezo ya Mpangaji	
Majina		Majina	
Namba Ya Kitambulisho		Namba Ya Kitambulisho	
Anwani ya Posta		Anwani ya Posta	
Namba Ya Simu		Namba Ya Simu	

3. Ardhi inayokodeshwa

Kipande cha ardhi kina kipimo cha _____ (ingiza vipimo katika mita) na mipake yake ni

(Eleza kipande cha ardhi kwa kutumia alama inayoonekana na ya kudumu)

4. Masharti ya kukodisha

Ada ya Kukodisha katika Ksh	
Masharti ya Malipo (eleza jinsi ya kulipa k.m, malipo ya awali, malipo ya baki)	
Muda wa Kukodisha	
Lengo la matumizi la mpangaji	

FOMU YA MKATABA WA KUKOSIDHA ARDHI - WADI YA ISUKHA-MAGHARIBI

Nakala zaidi za fomu hii zinapatikana katika Afisi ya Naibu wa Chifu/Chifu au Afisi ya Jumuiya ya Shibuye - CBO. Soko la Shinyalu

Uhuru wa matumizi kwa mpangaji (orodhesha kiwango cha uhuru na udhibiti kwa mpangaji)	
Uhuru wa Mmiliki (Orodhesha kiwango cha uhuru na udhibiti wa mmiliki)	
Mpangaji atatumia kipande cha ardhi kwa kipindi maalum na kurejesha kipande cha ardhi kwa mmiliki katika hali zifuatazo	

- Mkataba huu utakuwa wa kudumu kati ya Mmiliki na Mpangaji na marekebisho yoyote yataamaanisha uandikaji wa mkataba mpya.
- Uvunjaji wowote wa mkataba huu utatozwa faini ya Kshs. _____ kwa aliyevunja.
- Mizozo yoyote itakayotokana na makubaliano ya mkataba itawasilishwa kwa: _____

Imetiwa Sahihi na:

Mpangaji		Mmiliki
Sahihi:		Sahihi:
Alama ya Kidole(Gumba):		Alama ya Kidole(Gumba):
Majiina:		Majiina:
Namba Ya Kitambulisho:		Namba Ya Kitambulisho:
Namba Ya Simu:		Namba Ya Simu:
Tarehe:		Tarehe:

LAND LEASE AGREEMENT FORM - ISUKHA WEST WARD

More copies of this form can be obtained at the nearest Assistant Chief's, Chief's or Shibuye CBO Office in Shinyalu Market Centre

Mbele ya Mshahidi:

Shahidi (Mashahidi) wa Mpangaji		Shahidi (Mashahidi) wa Mmiliki	
Shahidi wa 1	Shahidi wa 2	Shahidi wa 1	Shahidi wa 2
Sahihi:	Sahihi:	Sahihi:	Sahihi:
IsharaYa kidole(Gumba)	IsharaYa kidole(Gumba)	IsharaYa kidole(Gumba)	IsharaYa kidole(Gumba)
Majina:	Majina:	Majina:	Majina:
Namba ya Kitambulisho:	Namba ya Kitambulisho:	Namba ya Kitambulisho:	Namba ya Kitambulisho:
Namba Ya Simu	Namba Ya Simu	Namba Ya Simu	Namba Ya Simu
Cheo:	Cheo:	Cheo:	Cheo:
Tarehe:	Tarehe:	Tarehe:	Tarehe:

Mbele ya:

Chifu/Naibu wa chifu/Mzee wa Kijiji

Sahihi: _____ Tarehe: _____

Majina: _____

Cheo: _____

FOMU YA MKATABA WA KUKOSIDHA ARDHI - WADI YA ISUKHA-MAGHARIBI

Nakala zaidi za fomu hii zinapatikana katika Afisi ya Naibu wa Chifu/Chifu au Afisi ya Jumuiya ya Shibuye - CBO. Soko la Shinyalu



Washiriki katika mkutano wa uzinduzi katika kanisa la PG katika kata ndogo ya Mukhonje © William Onura

Anwani/muhuri

Violet Shivutse, Director
Shibuye Community Health Workers CBO
on Tel: 0724 233930
Email: shibuyechw@yahoo.com